Toleo 35

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## TUMEITWA ILI TUTOKE GIZANI

*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.* —1 Petro 2:9


Ujumbe ambao wanadamu wamepata kutoka kiti cha enzi cha Mungu katika vizazi vyote vya kibinadamu ni ule ambao ungali wasikika na kutumika katika kizazi hiki chetu. Ujumbe huu wa kiungu unasema kwamba mwanadamu anahitaji kuacha giza la ulimwengu huu wa dhambi, na badala yake atembee katika mwangaza wa Mungu, mwangaza wa ajabu, wa kweli, na wa haki. Watu wengi wameingiza maisha yao katika tamaa za kimwili: uzinzi, usherati, ushoga, uchafu, ibada ya sanamu, chuki, mashindano, mabishano, wivu, mauaji, ulevi, burudani, na mengine mengi. Giza la kiroho linaendelea kusambaa kote nchini, huku watu wakimkataa Mungu na badala yake kufuata mipango yao ya kibinafsi ambayo inaongozwa na tamaa za mwili. Basi hebu tuseme hapa kwa njia ya wazi kabisa kwamba "watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu" (Wagalatia 5:19-21).

Watu wanaendelea kufanya jitihada za kunyamazisha sauti inayonena ndani mwao, sauti ya Roho wake Mungu, ambaye ndiye anawahakikishia swala hili, na wanajaribu kutoroka lawama na hukumu hiyo iliyomo ndani mwao, huku wakiendelea kufuatilia mambo ambayo hayafai, matendo ya uasherati na ya kufurahisha tamaa za kimwili, mambo ambayo ni ya muda mfupi. Watu wengine hata wanadai kwamba Mungu hayupo, na pia wanadai kwamba hakuna kipimo kilichokubalika cha kupima mema na mabaya. Nazo dini za kibinadamu zinajaribu kuunda injili ingine na kuipatia maana tofauti, ili kuwapa wanadamu nafasi ya kutenda dhambi, na wahubiri hawa wanakuwa wavumilivu kwa maovu yaliyomo kwenye mioyo ya wanadamu. Kwa kweli wanadamu walipenda giza kuliko mwangaza kwa sababu matendo yao ni maovu (Yohana 3:19).

Katika jamii yote watu wamefanywa wafungwa wa tabia mbaya ambazo zimewashika sana hivi kwamba hawana uwezo wa kuziacha, huku tabia bora zikitupiliwa mbali katika jamii, na giza la dhambi likiendelea kuenea. Na hata ingawa watu kadhaa wanasimama wima dhidi ya uchafu wa wakati tunaoishi, mara nyingi wao wenyewe huwa wanaongozwa na tamaa za kujitakia makuu, kiburi, na hata utajiri. Giza la kiroho la kila aina limewatenga wanadamu na Mungu, lakini ukweli wa mambo ni kwamba, mshahara wa dhambi ungali ni mauti.

Giza ni ukosefu wa mwangaza. Kwa mambo ya kiroho giza ni nguvu zinazotokana na mambo yote ambayo yako kinyume na Mungu, mambo ambayo huingia sehemu za ndani za mwanadamu; giza hilo humwathiri mwanadamu kimwili, kiakili, kihisia, na hata kiroho. Matendo ya kimwili na giza linaloletwa na dhambi, ambayo ndiyo mambo yanayopigiwa debe na wanasiasa na kuonyeshwa kuwa ni mema kupitia kwa vyombo vya habari na nyanja za burudani na hata katika michezo ni mambo ambayo yanaharibu maisha ya watu kibinafsi na kifamilia. Maisha ya dhambi na falsafa za kidunia si mambo ambayo yanaleta furaha, amani, au hali ya kutosheleka zaidi kwa maisha ya wanadamu; badala yake haya ni mambo ambayo hufanya watu kukata tamaaa, kuwa na upweke, kupoteza tumaini, na mwishowe kuwaletea wanadamu mauti, huku nafsi za wanadamu zikibaki na shauku la kupata kitu cha kukata kiu kilichomo ndani mwao.

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Giza ni ukosefu wa mwangaza. Kwa mambo ya kiroho giza ni nguvu zinazotokana na mambo yote ambayo yako kinyume na Mungu."


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tahariri | Mafundisho ya Biblia: Si Wa Ulimwengu | Si Wa Ulimwengu | Tumeitwa Ili Tuwe Watakatifu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

Sisi tunamshukuru Mungu kwa sababu kuna ukombozi wa kumtoa mtu dhambini na hata gizani kupitia kwa nguvu zake Yesu Kristo. "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7). Mwito ambao tumepata ni kwamba tunahitaji kutoka gizani na badala yake tuingie kwenye mwangaza wake wa ajabu. Mwangaza ndio ambao hufukuza giza, na mwangaza wa Yesu Kristo utafukuza nguvu za dhambi kutoka kwa nafsi zetu. Sisi wote tulishawahi kutembea gizani, na tukawa chini ya nguvu za mwili, lakini wale ambao wanaupokea mwito wa Mungu wanapata urembo wa mwangaza na hata amani. "Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima" (Yohana 8:12).



"Basi ni uwongo kutoka kwa Shetani kuwafanya watu kufikiri kwamba wanaweza kuchagua kuwa na giza kiasi fulani na pia mwangaza kiasi fulani."

Yesu alikuja ili "kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani" (Yohana 12:46). Basi ni uwongo kutoka kwa Shetani kuwafanya watu kufikiri kwamba wanaweza kuchagua kuwa na giza kiasi fulani na pia mwangaza kiasi fulani. Watoto wa Mungu wameitwa ili watoke gizani na kuenenda kama wana wa mwangaza, huku maisha yao yakidhihirisha mambo ambayo yamekubalika mbele za Bwana. Wao basi wako na jukumu sio tu la kuacha ushirika na matendo ya gizani, bali hata kuyakemea (Waefeso 5:8-11).

Wakati mtu amempokea Kristo na moyo wake wote na kutubu dhambi zake mwangaza wa Kristo unabadilisha maisha yake. Wakorintho wa Pili 5:17 ingali yasema ukweli kwamba: "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." Basi hakutakuwa na usemaji uongo, kuwahadaa watu, uasherati, uzinzi, chuki, au mambo mengine kama hayo. Nuru ya Kristo itamletea mtu huyo neema na tunda la Roho, tunda la upendo, amani, wema, n.k. (Wagalatia 5:22-25); na mtu huyo hataenenda tena katika tamaa za mwili, bali ataenenda kulingana na Roho. Kama wasafiri na wageni ulimwenguni huu watoto wa Mungu wameambiwa "ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho" (1 Petro 2:11) na watajitenga na ulimwengu na kuwa sehemu ya taifa takatifu.

Mwangaza wa Mungu humletea mtu uponyaji, mapatanisho, na hata amani, lakini ni lazima mtu ajijitenge kabisa na giza. "Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake . . . kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli" (1 Yohana 1:5-6). Hatuwezi kumpendeza Mungu na wakati huo huo kuongozwa na nia ya mwili, huku tukipendeza tamaa za kimwili (Warumi 8:5-8).

Ikiwa basi wewe unaishi gizani, hebu fungua moyo wako ili mwangaza wa Mungu uingie, na ili ufurahie baraka za kweli maishani mwako. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Enyi wa nyumba ya Israeli, njoni, twende katika nuru ya BWANA.* —Isaya 2:5

Kulingana na vile ulimwengu unaendelea kudidimia katika giza la dhambi ndivyo tofauti katika maisha ya jamii za sasa na za watu wa Mungu inastahili kuongezeka. Mwangaza wa kweli unaotoka kwa watu wa Mungu utazidi kung'ara kulingana na vile ambavyo giza la uovu litakavyozidi kuenea. Kama vile nabii Isaya aliwasihi watu wa kale wa Mungu, nami pia nawasihi: "Njooni, hebu twenende kwa nuru yake BWANA."

Somo la toleo hili la Ukweli wa Injili la muhula huu ni "Sio wa Ulimwengu Huu." Biblia inasema kwa njia iliyo wazi kabisa kuhusu haja ya watu wa Mungu kukataa ulimwengu huu na kumfuata Yesu kwa utakatifu. Somo la utakatifu ni somo kuu katika agano la kale na pia katika agano jipya; hata hivyo, viongozi wa kidini katika siku tunazoishi wanafutilia mbali kanuni za utakatifu kutoka katika mahubiri yao, na badala yake wanafundisha injili ya kijamii, injili ya kufanya watu kujihisi vizuri. Watu wengi, hata wengine wakijidai kwamba ni washirika wa Kanisa la Mungu, wanaishi maisha ya kidunia. Lakini hata kama ukweli huu haupendwi na watu wengi, ukweli dhabiti ni kwamba, utakatifu si jambo la mtu kuchagua kuwa nao au la; utakatifu ni jambo la lazima kabisa ikiwa sisi tunataka kumpendeza Mungu na kufanya Mbinguni kuwa nyumbani mwetu.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Watakatifu wanastahili kudhirisha utakatifu katika kila fani ya maisha yao, huku wakiwa mabalozi bora wa Yesu Kristo. Lakini utakatifu wa kweli ni zaidi ya matendo yanayoonekana na watu; utakatifu wa kweli ni usafi wa ndani ambao unatokana na uwepo wa Roho Mtakatifu, ambaye anadumu moyoni mwa muumini. Mtu akijitolea kabisa kwa Mungu jambo hili litamfanya kuachana na vitu na roho ya ulimwengu wa sasa. Kusema kweli utakatifu ni hali ya moyo wa mtu.

Ni shauku langu kubwa kuona watu wengi zaidi wakiokoka na kumkubali Bwana Yesu; lakini moyo wangu pia una huzuni nyingi kutokana na kuona jinsi watu wengi wanaojiita Wakristo walivyo na mwelekeo wa kutojali, na pia kutoshughulishwa na uovu na athari zilizomo ulimwengu wa sasa. Rafiki zangu, ukweli wa mambo ni kwamba kumuishia Mungu ni jambo ambalo lingali linatubidi tuachane na ulimwengu huu na kuishi maisha ambayo yanalingana na wimbo ule unaosema: "Nimeacha ulimwengu wote ili kumfuata Yesu."

Vijana wengi wanafanya maamuzi kuhusu maisha yao kwa maswala ya kazi watakayofanya, elimu watakayosoma, watamwoa nani, au watavaa vipi n.k. kwa misingi ya mambo ambayo yanatiliwa umuhimu na ulimwengu, na kwa ajili ya malengo ya kilimwengu. Lakini mali yote na heshima na kiburi ya kilimwengu ni mambo ambayo hayana maana yoyote kwa Mungu Mtakatifu, na ni mambo ambayo hayatamletea mtu utakatifu, aidha katika ulimwengu huu, au hata katika ulimwengu unaokuja. Hebu basi tuweke rasilmali yetu kwa mambo ya kiroho na kutafuta mambo ambayo ni mema, mambo ambayo yataleta manufaa kwa ajili ya hali bora yetu ya kiroho, na ya wale wanaotuzunguka. Tangu jadi watu (wa kweli) wa Mungu wamekuwa ni wachache, na jambo hilo si tofauti katika kizazi chetu. Tunapoishi maisha matakatifu, matendo, maneno, na hata mavazi tutakayovaa yatakuwa tofauti na yale ya watu wa dunia. Basi mambo ambayo tunayojishughulisha nayo yanahitaji kuwa yale ambayo yanampendeza Baba yetu, ambaye ni Mungu Mtakatifu, na maisha yetu yatahitaji kudhihirisha haki yake. Lakini ukweli ni kwamba si watu wengi wako tayari kuupokea ukweli huu bila kutoa pingamizi. Maisha yetu hayastahili kupimwa kulingana na misingi ya ulimwengu huu, bali kwa kulingana na viwango vya utakatifu ambavyo viko dhahiri katika Neno la Mungu.

Ewe mtoto wa Mungu, hatuwezi kamwe kuishi kulingana na misingi ya ulimwengu huu. Basi hebu tukumbatie utakatifu huo na kuyatoa maisha yetu mhanga kwa Mungu. Hebu tuweke kando matendo ya dhambi pamoja na falsafa za kilimwengu na tujitenge kutokana na athari ambazo hufanya mtu kuishi kulingana na njia za kilimwengu. Hebu tuwe watu ambao akili zetu zimeelekezwa mbinguni na tuweze kumtukuza Mungu kwa utakatifu.

Michael W. Smith

Januari 2021.

MTU AKIJITOLEA KABISA KWA MUNGU JAMBO HILI LITAMFANYA KUACHANA NA VITU NA ROHO YA ULIMWENGU WA SASA. KUSEMA KWELI UTAKATIFU NI HALI YA MOYO WA MTU.

# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: SI WA ULIMWENGU



**Somo la Maandiko:** *Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.* —Yohana 17:14-16

**Muhstasari:** Wakristo wameitwa ili watoke gizani la ulimwengu na kuishi maisha matakatifu, huku wakitembea kulingana na mwangaza wake Kristo. Wakristo wanastahili kujivua athari za kilimwengu na kuishi maisha ya kila siku kwa kumtukuza Mungu kwa kila jambo.

### I. Kuitwa kutoka Gizani

A. 1 Petro 2:9-11 Kuitwa kutoka gizani.
B. Wagalatia 5:16-25 Watu watendao matendo ya kimwili hawataingia Mbinguni.
C. Yohana 3:19 Watu wanapenda giza kuliko nuru.
D. 1 Yohana 1:5-7 Mtu hawezi kuwa na ushirika na Mungu na wakati huo huo kukaa gizani. Damu ya Yesu yatusafisha dhambi zote.
E. Yohana 8:12 Wafuasi wa Yesu hawatatembea gizani.
F. Yohana 12:46 Wanaoamini hawatakaa gizani.
G. Waefeso 5:8-11 Myakemee matendo ya giza.
H. 2 Wakorintho 5:17 Katika Kristo mambo ya kale yamepita.
I. Warumi 8:5-8 Kufuata nia ya mwili humletea mtu kifo.

### II. Si wa Ulimwengu

A. Yohana 17:14-16 Wanafunzi wa Kristo si wa ulimwengu
B. Yohana 15:18-19 Niliwachagua kutika ulimwengu. Ulimwengu utawachukia.
C. 1 Yohana 3:1 Ulimwengu haututambui.

### III. Msiipende Dunia

A. 1 Yohana 2:15 Msiipende dunia.
B. 1 Yohana 2:16 Tamaa haitoki kwa Baba.
C. Wakolosai 3:12 Tafuteni yaliyo juu.

### IV. Nguvu ya Ulimwengu

A. 2 Wakorintho 4:4 Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini.
B. Wakolosai 2:8 Kutekwa na elimu ya bure na kwa madanganyo matupu.

### V. Hekima ya Dunia

A. 1 Wakorintho 3:18-19 Hekima ya dunia ni upumbavu kwa Mungu.
B. 1 Wakorintho 1:18-25 Upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu.

### VI. Maonyo

A. 2 Timotheo 2:4 Kutojitia katika shughuli za dunia.
B. Warumi 12:1-2 Kutofuatisha namna ya dunia.
C. Yakobo 4:4 Urafiki wa dunia ni uadui wa Mungu.
D. Yakobo 1:27 Kujilinda na dunia pasipo mawaa.

### VII. Mazao

A. Mathayo 16:24-26 Atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake?
B. Wagalatia 6:7-8 Apandacho mtu, ndicho atakachovuna milele.

### VIII. Kuitwa ili Kuwa Watakatifu

A. 1 Petro 1:15-16 Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu.
B. 1 Wakorintho 6:18-20 Mtukuze Mungu katika miili na roho.
C. Waebrania 12:24 Bila utakatifu hakuna mtu atakayemwona Mungu.

**Tamati**

*Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa.* —2 Petro 3:11

# Si Wa ULIMWENGU

**Daima wafuasi wa kweli wa Kristo watatenganishwa na kuwa tofauti na ulimwengu huu kwa maadili wanayoishi nayo, kusudi za maisha yao, tabia zao, kwa mambo yao ya kiroho, mavazi, na hata jinsi wanaendesha shughuli zao za kila siku. Lakini pia kuna watu ambao hujidai kuwa ni Wakristo lakini wanaishi maisha ambayo ni mamoja na ulimwengu, maisha ambayo yanakiuka kanuni za Yeye ambaye wanadai kuabudu na kutumikia.**



Hata ingawa makanisa yamejaa watu ambao bado wanapenda ulimwengu, na ambao wanajidai kwamba wao wanapenda Mungu, Kanisa la kiungu (la Mungu) limejaa watu ambao wanapenda Mungu kwa mioyo yao yote, na ambao wamejitolea kwa Kristo na kwa malengo yake kuliko jambo lingine lote. Lakini hata ingawa Watoto wa Mungu ni wasafiri humu duniani wao wangali wanahitaji mahali pa kufanya kazi, mashule ya kuhudhuria, manyumba ya kuishi, na hata pesa za kuwawezesha kununua kile ambacho wanahitaji. Lakini kamwe wao hawatafuti mambo ya thamani ya dunia hii, na badala yake lengo la maisha yao ni kumpendeza Mungu kila siku kwa upendo wa mioyo yao, nguvu za miili yao, na hata mali yao ya hapa ulimwenguni.

## Wamo Ulimwenguni lakini Si wa Ulimwengu

Ukweli mkuu kuhusiana na haja ya sisi kumuishia Mungu unapatikana katika maombi ambayo Kristo aliomba kwa niaba ya wanafunzi wake "Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu" (Yohana 17:15-16). Halikuwa lengo lake Mungu kwamba watu wake wajitenge kutokana na jamii zao na kuanzilisha vijiji na makao ya wao kuishi kama watakatifu. Badala yake lengo lake Yesu kwa watoto wake ni kwamba wao waenende ulimwenguni kote na kuruhusu mwanga wa ukweli kung'aa kabisa kwa jinsi ambavyo wanaishi maisha matakatifu, maisha tofauti, maisha ambayo yako huru kutokana na uovu na athari ambazo zimewazunguka.

## Maana ya Ulmwengu

Ni jambo muhimu sisi kuelewa wito na matakwa ya sisi kutenganishwa na ulimwengu. Neno "ulimwengu" linatumika kwa njia tofauti tofauti katika Maandiko. Ulimwengu waweza kuchukuliwa kuwa ni dunia ambayo Mungu aliumba; laweza pia kutumika kumaanisha wanadamu kwa jumla, kama vile kusema "Mungu aliupenda ulimwengu"; lakini pia neno ulimwengu linaweza kumaanisha sheria, kanuni, na mambo ambayo huongoza watu ambao wangali hawajakombolewa, na malengo ambayo wao hufuata maishani mwao. Kusema kweli hii maana ya mwisho ndio ambayo Kristo alimaanisha alipotangaza kwamba wanafunzi wake "si wa ulimwengu." Watu ambao wanaishi na kutafuta mambo ambayo yanayongoza mienendo ya ulimwengu na walimwengu sio wafuasi wa Kristo, kwa maana Wakristo si wa ulimwengu huu.

## Kuchukiwa na Ulimwengu

Kwa njia ya wazi kabisa Yesu alisema kwamba jamii kwa jumla itawachukia wanafunzi wake, kwa sababu wao si wa ulimwengu huu. "Naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia" (Yohana 15:18-19). Watu wa ulimwengu huu wanapenda wenza wao, lakini wao huchukia matakwa ya utakatifu, na pia wanachukia maisha ya utauwa. Basi kulingana na Maandiko kama mtu anapendwa na ulimwengu basi yeye ni mmoja na walimwengu, na ni kusema kwamba yeye haishi maisha ambayo ameitiwa ya kutoka ulimwenguni. Wanafunzi wa Yesu wanaishi kulingana na sheria ya utakatifu, sheria ambayo ni tofauti na roho na shauku ya watu wa kimwili ambao bado hawajaokoka. "Kwa sababu hii ulimwengu hautuambui, kwa kuwa haukumtambua yeye" (1 Yohana 3:1).

## Msiipende Dunia

Hata ingawa kumekuwa na jitihada za kudhoofisha utakatifu wa kweli, kwa njia ya watu kuchanganya na kuingiza kanuni za dunia katika Ukristo, Maandiko yako wazi kabisa: "Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake" (1 Yohana 2:15). Shauku za mioyo ya Wakristo zinahitaji kuwa kwa Mungu, na kamwe wao hawastahili kuongozwa na mambo au roho wa kilimwengu, roho ambaye sio wa utakatifu. Mtoto wa Mungu anastahili kujitenga dhidi ya athari za kilimwengu, na kujilinda dhidi ya matamanio na shauku za dhambi, kiburi, tamaa, kupenda anasa, na kujitafutia heshima za kilimwengu. Upendo wa ulimwengu na upendo wa Mungu ni mambo ambayo hayaambatani, na kamwe hayawezi kudumu pamoja.

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

"Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia" (1 Yohana 2:16). Maandiko yamesema waziwazi kuhusu mambo ambayo ni ya kilimwengu, ambayo hayatokani na Baba yetu. Tamaa za mwili ni shauku la kujipendeza kimwili kwa njia ya hisia ambazo sio safi; jambo hili huhusisha matumizi ya madawa ya kulevya, pombe, ulafi, uasherati, n.k. Ulimwengu umejaa tabia ambazo kamwe hazikubaliki katika jamii. Kuvaa mavazi ambayo yanambana mtu na kuonyesha mwili wake hadharani ni jambo la kilimwengu na ambalo liko kinyume na yale yanayofundishwa katika Biblia kuhusiana na haja ya Mkristo kuishi maisha yanayoongozwa na viwango vya wastani vya maisha, na pia haja mtu wa Mungu kuishi kwa urahisi wa maisha. Kujipondoa na kuvaa vipuli pia ni mambo ambayo yanaambatana na roho wa ulimwengu, na pia ni mambo ambayo huchochea tamaa za macho. Shauku za kuvaa a nguo za bei ghali na za kifahari, kuishi nyumba kubwa kubwa na kuendesha magari ya bei ghali ya "kuwaringia" watu ni mambo ambayo yanatokana na kiburi, na kamwe hayatokani na Baba wetu. Kiburi cha maisha pia kinahusisha roho ya mtu kujitakia makuu, na yenye kutaka heshima na kutambuliwa na mwanadamu. Jambo hili pia linahusu watu kupenda kupata sifa za watu, na heshima ambayo hutokana na mali na utajiri wa kilimwengu.

Tamaa hizi na malengo na shauku za kilimwengu ni mambo ambayo hayalingani na mtu kwenda pamoja na Mungu kwa njia ya unyenyekevu na upendo. Lakini ikiwa kimaumbile mtu anavutiwa sana na mambo haya, kuna neema inayopatikana ambayo itamwezesha kushinda, ili kwamba yeye aweze kuishi maisha ambayo yanampendeza Kristo. "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi" (Wakolosai 3:1-2).

## Nguvu na Hekima ya Kidunia

2 Wakorintho 4:4 inatufundisha kwamba "mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini." Kuna nguvu nyingi na uwezo katika mambo na roho za kidunia. Watoto wengi wa Mungu wameanguka na kuacha wokovu wao kwa njia ya wao kujiingiza katika mambo ya ulimwengu, na hata wakafikia kupoteza upendo wao kwa Mungu. Michezo, muziki, burudani, na mitindo ya mavazi, ni baadhi ya mambo na miungu ya dunia hii ambayo watu huabudu, kwa sababu haya ndiyo mambo ambayo wanadamu wanapenda, mambo ambayo huchukua wakati wao, na kuongoza jinsi wanatumia pesa zao. Lakini nguvu kamili za ulimwengu huu hazipatikani katika mambo haya, bali inapatikana katika falsafa na itikadi za kilimwengu. "Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo" (Wakolosai 2:8).

Watoto wa Mungu wanastahili kuwa macho, kwa maana wasipokuwa macho wao watavutiwa katika akili zao ili polepole watoke nje ya utakatifu wa kweli wa maisha yao ya kila siku. Wakristo wanaweza kupoteza utakatifu wao kwa njia ya kuwasikiliza watu ambao ni wa kimwili, na ambao hawamchi Mungu. Waalimu na viongozi wa kidini ambao bado hawajakombolewa hujidai kwamba wao wana elimu zaidi na uelewaji wa hali ya juu, na pia kudai kwamba wao wana akili timamu sana, na mwangaza zaidi, na kwa njia hiyo wanaanza kupuuzilia mbali utauwa, na kufundisha watu wafungue akili zao na kukubali mambo ambayo yako kinyume na maisha ya utauwa.

Lakini katika 1 Wakorintho 3:19 mtume Paulo aliandikia kanisa la Korintho na kuwaonya: "Maana hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu. Kwa maana imeandikwa, Yeye ndiye awanasaye wenye hekima katika hila yao." Mahubiri kuhusu msalaba ni upumbavu kwa ulimwengu, lakini ni nguvu za Mungu; nao "upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu" (1 Wakorintho 1:18-25). Ni nani ambaye wewe Mkristo unasikiliza ili akufundishe na kukuongoza? Lengo kuu la jamii za sasa ni kuwavutia watu ili waachane na utakatifu. Basi wewe mtoto wa Mungu kaa macho!

## Maonyo

Kuna haja ya sisi kutoa onyo kubwa kwamba hata ingawa sisi tunaishi ulimwenguni, kamwe tusiwe watu wa ulimwengu. "Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia" (2 Timotheo 2:4). Basi sisi hatuhitaji kujihusisha katika siasa na milengo ya kijamii. Ni jambo rahisi kwa nia ya kimwili kuingi kati katika "malengo bora" na kuharibu roho na mwelekeo ambao mbeleni ulikuwa umetakaswa kwa Mungu.

Kanisa la Kirumi lilipata himizo kwamba "msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu" (Warumi 12:1-2). Basi tunahitaji pia kutoa himizo hilo kwa kanisa la leo. Nia za watu wengi zinahitaji kubadilishwa, hii ni kwa sababu kuna Wakristo wengi ambao wanafuatisha mambo ya dunia kwa malengo ya maisha yao, roho zao, na hata katika mavazi yao; hili ni jambo ambalo halikubaliki kwake Mungu. Kwa nguvu na kwa ukweli kabisa Yakobo 4:4 inasema kwamba: "kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu." Hata ingawa kuna mafundisho mengi ambayo yanafundishwa na viongozi wa kidini ambao wamejiingiza katika mambo ya kidunia, dini ya kweli ingali ile ya "kujilinda na dunia pasipo mawaa" (Yakobo 1:27).

Ni ombi langu kwamba macho ya vipofu wa kiroho yatafunguliwa ili wao waweze kuona hatari za ulimwengu na pia kuona urembo wa utakatifu. Wewe msomaji wangu hebu chunguza maisha yako kwa misingi ya Neno la Mungu. Je, maisha yako yamejaa dosari za ulimwengu, au dhamiri yako iko safi mbele zake Mungu na unaweza kusema kwamba, "Mimi sio wa ulimwengu huu kama ambavyo Kristo hakuwa wa ulimwengu huu?" Je, wewe u tayari kuwa tofauti na ulimwengu huu, kuwa tofauti na familia yako, na hata kuwa tofauti na marafiki zako, na kufanya msimamo wako kuwa ni ule wa kumfuata Yesu? Je, utafaidika nini kupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yako (Mathayo 16:24-26).

Punde si punde ulimwengu huu utapita, na wale ambao wanafuata njia zake watapatwa na kifo na adhabu ya milele; lakini maisha ya milele yanamsubiri mtoto wake Mungu ambaye "si wa ulimwengu huu" kupitia kwaYesu Kristo. ■



# Tumeitwa ili tuwe WATAKATIFU

Kumwishia Mungu kwa utakatifu ni jambo ambalo hutosheleza sana maishani. Pia kutumika katika ule "Wajibu Mkuu" wa Mkristo, na kushiriki mpango wa Mungu maishani mwetu ni jambo linalomletea mtu furaha kuu, na pia kumwezesha kutumia maisha yake kikamilifu. Ingawa kuna barabara nyingi ambazo mtu anaweza kupitia maishani, ni moja tu ambaye inamwongoza mtu hadi kwa uzima wa milele. Ni kweli kwamba njia ni nyembamba na ni wachache huipitia, lakini ukweli kabisa ni kwamba hii ndio njia bora. Mtu akitembea katika barabara kuu ya utakatifu ataweza kupata pumziko la kweli na roho yake itapata amani, kwa maana ni katika uwepo wake Bwana ndipo mtu hupata tosheleko kamili. Kwa kweli tunaweza kumwona Bwana kwa kuishi maisha matakatifu, kwa maana yeye ni Mungu mtakatifu. Lakini wengi hujaribu kumpata Mungu kwa kuchanganya roho ya dunia na ya kile kinajulikana kama kanuni bora za kuishi maisha haya ya kisasa. Hili ni jambo ambalo linadhihirika kupitia kwa muziki wa "kidini" na ibada za sifa za kidunia ambazo hutumia maneno ya kiungu na kuweka ndani yake muziki wa kidunia ili kuvutia hisia za washirika wa kanisa. Lakini ushirika wa kweli na Mungu haupatikani katika mchanganyiko huu, bali hupatikana katika usafi na utakatifu.

Kutoka mwanzo lengo lake Mungu lilikuwa kupata watu ambao wako tofauti na pia ambao ni watakatifu, watu ambao wamejitolea kumwabudu Yeye. Undani wa mafundisho yake Kristo unahusu utakatifu. Yeye alifundisha wanafunzi wake jinsi ya kudhihirisha utukufu huo wa Mungu kwa ulimwengu ambao umepotea. "Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (1 Petro 1:15-16). Sisi tumeitwa ili tuwe na ujuzi wa kuishi maisha matakatifu, kwa maana bila utakatifu huo hatuwezi kuishi kwa upatanisho na Mungu. Utakatifu wa kweli ambao unapatikana kutokana na uwepo wake Kristo ndio unatuwezesha na kutupatia nguvu za kuishi kwa njia ambayo inampendeza Bwana. Basi tunastahili kuishi maisha matakatifu katika kila nyanja ya maisha yetu. Lakini maana kamili ya utakatifu sio tu "kutakaswa" bali pia ni "kukamilika kwa njia zote." Mkristo anastahili kuishi kwa roho na nia moja kwa nje na ndani. Maisha ya Mkristo yanahitaji kuwa na lengo moja kutoka ndani ya roho yake hadi kwenye matendo yake.

> "Maisha ya Mkristo yanahitaji kuwa na lengo moja kutoka ndani ya roho yake hadi kwenye matendo yake."

1 Wakorintho 6:20 inasema kwamba: "Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu." Kumtukuza Mungu ndilo jambo kuu ambalo linaguza kila sehemu ya maisha yetu: kuanzia motisha ya maamuzi tunayofanya, hadi maneno tunayonena, mielekeo ya mawazo yetu, na hata mavazi tunayovaa. Watoto wa Mungu wameitwa ili kila siku wawe wa kumtukuza Mungu kwa kila njia.

Adui yetu Shetani anajaribu kutuonyesha kwamba maisha ya utakatifu ni maisha ya kuishi kifungoni. Eti ni maisha ya kuambiwa "Huwezi fanya hivi, huwezi fanya kile, huwezi kwenda huko, na huwezi kusikiliza hayo" n.k. Lakini adui huyo ni mwongo. Utakatifu ni jambo la kumweka mtu huru, sio la kumweka kifungoni. Utakatifu ndani yake Kristo unamwezesha Mkristo kuwa mtu huru kutokana na nguvu za ulimwengu ambazo ndizo huongoza wanadamu na kuwashika mateka. Lakini wokovu na utakatifu wa kweli ndio ambao hutukomboa kutokana na woga na mateso. Kama ambavyo wimbo mmoja umesema, hili ni jambo ambalo "hutukomboa kutokana na chuki, wivu, na mabishano." Utakatifu huu ni jambo ambalo linahusu sana kile ambacho tunaweza kufanya ndani yake Kristo, badala ya kile ambacho hatuwezi kufanya ulimwenguni.

Kuishi maisha matakatifu ndio wito mkuu, na ni jambo ambalo linatwezesha kuisha maisha ambayo ni tofauti kabisa na wanadamu wanaotuzunguka. Kuitikia wito huu wa kuwa tofauti na ulimwengu ni jambo ambalo linahitaji ujasiri na ushujaa, lakini malipo yake ni ya milele. Basi ni jambo muhimu kabisa mtu kuitikia wito wa utakatifu kwa sababu bila huu "hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao" (Waebrania 2:14). ■

> "MAANA MUNGU HAKUTUITIA UCHAFU, BALI TUWE KATIKA UTAKASO."
> 1 WATHESALONIKE 4:7


JE, WAJUA?

Kulingana na maandishi yale ya circa, ya hapo mwaka 210 BK, ambayo yaliandikwa na Tertullian: "Kama wewe wajiona kuwa ni Mkristo, basi kuwa tofauti na kafiri. Mrudishie kafiri maoni yake kuhusu maisha! Ikiwa kwa kweli kafiri huyu hajifunzi kutokana na mawazo yako kuhusu maswala ya maisha, inawezekanaje wewe kumtegemea kiongozi huyu kipofu kama wewe tayari unayo macho yako mwenyewe? Ni kwa nini uvalishwe nguo na mtu ambaye yu uchi kabisa, ikiwa wewe tayari umemvaa Kristo?"

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# MJUMBE WA HAKI

*Wala [Mungu] hakuuachilia ulimwengu wa kale, bali alimhifadhi Nuhu, mjumbe wa haki, na watu wengine saba, hapo alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasiomcha Mungu.* —2 Petro 2:5



Huku akiwa mtiifu kwa agizo la kiungu alilopata Nuhu alifanya bidii kwa miaka mingi ili kujenga safina. Safina hii ilikusudiwa kuokoa watu kutokana na gharika ambayo ingewaangamiza waovu wote kwa sababu ya hukumu ya Mungu juu yao. Hata ingawa Nuhu alichekelewa na kukejeliwa, yeye aliendelea kudumisha msimamo wake kwa Mungu na kamwe hakufuata msukumo wa jamii yake. Basi akasimama peke yake huku akiamini kwamba neno la Mungu lilikuwa kweli. Ndiposa "aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani" (Waebrania 11:7).

Mwanzo 6:9 inatwambia kwamba "Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu." Ni dhahiri kwamba Nuhu hakuficha imani yake ndani ya moyo wake bali alikuwa mjumbe au mhubiri wa haki. Yeye alihubiri ukweli na haki kupitia kwa matendo yake na maneno yake. Lingekuwa jambo rahisi kabisa yeye kunyamaza na kuendelea na shughuli zake, lakini Nuhu aliumwa na uovu huo wa wanadamu ndiposa akahubiri haki kwa watu wa kizazi chake ili kuwapa nafasi ya wao kunyenyekea na kutubu dhambi zao kabla ya hukumu ya Mungu kuwafikia.

Kuna haja kubwa ya kuwe na wahubiri wa haki siku tunazoishi wanaohubiri kwa kizazi cha sasa ambacho ni kiovu. Wahubiri wengi wanahubiri mambo ya kufanya watu kujihisi vizuri, huku wanadamu hawa wakiendelea kudumu dhambini mwao. Wao wanafundisha mambo ambayo ni rahisi watu kusikia na kukubali. Lakini Mungu ni mtakatifu na wahudumu wake wanahitaji kuwa watu watakatifu na wanaohubiri haja ya watu wa Mungu kutengwa na kuachana na uovu na roho ya dunia hii. Huenda mhubiri wa utakatifu akakejeliwa, akadhihakiwa, na hata kuteswa. Na kuna watu ambao watagoma kuja kanisani humo kwa sababu wamekwazwa na mahubiri hayo. Lakini ni bora zaidi watu wakwazwe katika maisha haya ya sasa huku kukiwa wangali na nafasi ya wao kutubu, badala ya wao kukwazwa milele wakati hukumu ya Mungu itakapofika, wakati ambapo hawatakuwa na nafasi ya kupata ukombozi.

Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku ya hukumu ya mwisho. Watakatifu wataokolewa, na waovu watatengwa kabisa kwa njia ya kifo cha milele. Ni ombi langu kwamba Mungu atawapatia wahudumu wote wa Injili ujasiri wa Roho Mtakatifu ili waweze kutangaza ukweli wote kuhusiana na utakatifu bila kizuizi chochote, kwa maana ujumbe huu ndio utaziokoa roho za wanadamu. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana